موقف

الشيعة الإمامية الاثني عشرية

من الصوفية

MSIMAMO WA SHIA

IMAMIYAH ITHNA ASHER

JUU YA MASUFI

**1438 - 2017**

# موقف
# الشيعة الإمامية الاثني عشرية
# من الصوفية

# MSIMAMO WA SHIA IMAMIYAH ITHNA ASHER JUU YA MASUFI


بقلم

عبدالله بن محمد

MWANDISHI

ABDALLAH BIN MOHAMMAD

بسم الله الرحمن الرحيم

# YALIYOMO

UTANGULIZI . . . 7
MAKOSA YA KIITIKADI KATI YA MASUFI NA SHIA IMAMIYAH. . . . 12
MSIMAMO WA SHIA AL-IMAMIYAH KUHUSU SUNNA ZA MTUME . . . 18
MSIMAMO WA SHIA IMAMIYAH KUHUSU SWAHABA WA MTUME . . . 22
MSIMAMO WAO KWA MAMA WA WAUMINI . . . 26
DUA YA MASANAMU MAWILI YA KIQURAYSH. . . . 29
MSIMAMO WA SHIA AL-IMAMIYA AL-ITHNAA'SHARIYAH KWA MASUFI . . . 30
MASUFI MBELE YA MASHIA NI MAYAHUDI WA UMMA HUU NA NI WAPOTOFU KULIKO MAKAFIRI NAO NI WATU WA MOTONI NA AMALI ZAO NI AMALI ZA WATU WAOVU . . . 33
MSIMAMO WA MAIMAMU WA KISHIA KWA MASUFI . 35
MSIMAMO WA IMAMU AL-SADIQ JUU YA MASUFI NA HUKUMU KWAMBA NI WATU WA ITIKADI MBOVU . . . 36
MSIMAMO WA IMAMU MUSSA BIN JAAFAR KWA TASAWUF. . . . 37
MSIMAMO WA IMAMU AL-RIDHA JUU YA MASUFI NA HUKUMU YAKE KWAO KUWA NI WATU WA UPOTOFU NA WAJINGA NA MWENYE KUWAPINGA NI SAWA KWAMBA AMEPIGANA JIHADI DHIDI YA MAKAFIRI PAMOJA NA MTUME ﷺ . . . 39

MSIMAMO WA IMAMU AL-HAADI JUU YA MASUFI NA HUKUMU YAO KWAMBA NI MANASARA NA WAMAJUSI WA UMMA HUU . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . **41**
MSIMAMO WA IMAMU AL-ASKARY JUU YA MASUFI . **43**
IJMAI YA SHIA IMAMIYAH YA UBATILI WA MASUFI NA KUFURU YA WAFUASI . . . . . . . . . . . . . . . . . . . **44**
MSIMAMO WA MAULAMAA WA KIIMAMIYAH WALIOWARUDI MASUFI NA KUWAITA MAKAFIRI NA WAPOTOFU . . . . . . . . . . **46**
HAIJUZU KUJINASIBISHA NA TASAWUFI ISIPOKUWA KWA HALI YA KUFANYA TAQIYA. . . . . . . . . . . . . . . . **54**
MWISHO . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . . **56**
ORODHA YA VITABU MUHIMU DHIDI YA SHIA . . . . . **58**
MITANDAO MUHIMU AMBAYO TUNASHAURI KUPERUZI KATIKA KUWARUDI RAFIDHWA ITHNA ASHARIA . . . . . . . . **60**

بِسْمِ ٱللَّهِ ٱلرَّحْمَٰنِ ٱلرَّحِيمِ

Sifa zote njema anastahiki Allah, na rehema na amani zimfikie bwana wetu Mohammad, ambaye ni Mjumbe na rehema kwa walimwengu wote, amani ya Allah imfikie Yeye, jamaa zake na swahaba zake, ama baada ya hayo:

Sio siri kwa watafutao elimu na wajishughulishao na masuala ya Kishia, (kuujua) msimamo wa Shia Ithnaa Asher dhidi ya wanaowapinga, na kwamba Shia humkufurisha na kumpotoa kila anayewapinga, bali hata makundi ya Kishia kama Zaidiyah, Ismailiyah na makundi mengine ya Kishia. Kwa mtazamo wa Shia Imamiyah makundi yote hayo ni makafiri[1]

Mashia wa Ithnaa Asher wanajiona wao ndio kundi okovu na lililosalimika kama wanavyothibitisha wanazuoni wa Kishia:- An Nobakhtiy, Al-qummiy, Al-kasshiy na wanazuoni wengine wa Imamiyah. Na hii si mada ya ujumbe wetu huu.

Swali: Ni kwa nini nimetenga ujumbe kuhusu msimamo wa Shia Ithnaa Asher na Masufi kwenye ujumbe unaojitegemea?

---

[1] Rejea kitabu (Asshia'h Al-imamiyah Al-ithnaa Ashariyah watakfiyruhum liu'mumil Muslimiyn) Cha Abdullahi Assalafiy, na Kitabu (Dhwahiratut Takfiyr fiy Madh-habi Shia'til Imamiyah Al-ithnaa Ashariyah), Cha Dr, Abdur Rahman Dimashqiyah, na Kitabu (Al-fikrut Takfiyriy I'nda Shia'h Haqiyqatun Am Iftiraa) Cha Mhakiki Abdul Malik As Shafi'y.

Jibu la hili ni kuwa: Watu wengi waufanyao Usufi kuwa ndio mfumo na njia yao ya ibada, hawaijui hadhi na nafasi yao mbele ya Shia Imamiyah na wafuasi wao.

Na kabla sijaanza kuonesha niliyo nayo, nitavinjari pamoja nanyi kwenye tunzi za wanazuoni wa Kishia Imamiyah (ili muone) jinsi wanavyo waumbua Masufi.

Anasema Al-hurru Al-a'miliy katika kitabu chake: ''Risalatul Ithnaa A'shariyah fir Raddi A'laas Suufiyah'': ''Katu hajawahi Shia yeyote kuwa Sufi, kama ilivyo wazi kwa wanaofuatilia vitabu vya hadithi, wapokezi na wanaojishughulisha na fani hii, na Usufi na Masufi kwenye vitabu vya Shia hawajatajwa kwa wema wala kwenye maneno ya Maimam (amani iwe juu yao), isipokuwa hutajwa kwa uovu, na (Maimam) katika kuwarudi Masufi wametunga vitabu kadhaa, baadhi yake wamevitaja kwenye fahirisi ya vitabu vya Shia''[1].

Aliyehakiki Kitabu ametaja majina ya vitabu hivyo:-

1. Ar Risalatul Ithnaa A'shariyah fir Raddi A'laas Sufiyati - Cha Al-huru Al-'amiliy.

2. Ar Raddu A'laas Sufiyati cha Mhakiki Al-qummiy.

3. Ar Raddu A'laas Sufiyati Cha Al-maulaa Ismaili ibn Mohammad ibn Husein Al-mazindraniy, mashuhuri kwa jina la Al-khawajuiy.

4. Ar Raddu A'laas Sufiyati cha Asseyyid A'dhwam Aliy Al-bankoriy.

---

[1] Ar Risaalatu Al-ithnaa A'shariyatu fir Radi A'laa Sufiyah uk 12

**5.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, kilichodondolewa kutoka kwenye Kitabu Hadiqatu Shia (Cha Al-dabiriy) kilidondolewa na waliyoishi naye.

**6.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha Kifursi, cha baadhi ya watawala wa enzi za Fat-h Aliy Shah.

**7.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha kifursi, cha baadhi ya wanazuoni (Muhamad Rafii Atbriyziy -musswada- unaopatikana kwenye Maktaba ya mwanazuoni Aseyid Mahdiy Al-huseyniy Al-azourdiy.

**8.** Ar Raddu A'laas Sufiyati Cha Al-amir Muhamad Taqiyu Al-kashmiriy.

**9.** Ar Raddu A'laas Sufiyati Cha Al-maulaa Hasan ibn Muhamad Aliy Al-yazdiy.

**10.** Ar Raddu A'laas Sufiyati Cha Asseyid Dal-daar Aliy Al-majaz kutoka kwa Bwana wetu Seyyid Al-ulum.

**11.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha Al-haj Muhamad Aridhwaa Al-qaz-winiy.

**12.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha Al-maulaa Muhamad Twahir ibn Husein As Shiraziy An Najafiy Al-qummiy.

**13.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha Sheikh Aliy ibn Al-mirza Fadhlullahi Al-mazandraniy.

**14.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha Asseyid Muhamad Aliy ibn Muhamad Mumin Twabaa twabaiy.

**15.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha Kifursi Cha Aseyid Fadhil ibn Seyyid Qadhwiy Al- hashimiy.

**16.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha Sheikh Muhamad ibn Aliy Al-qutwayfiy.

**17.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha Al-maulaa Mutwahir ibn Muhamad Al-miqdadiy Farisiy.

**18.** Ar Raddu A'laas Sufiyati, Cha Kifursi, Cha Al-maulaa Fat-hallah Al-mutakhallis (Wafaaiy), na vitabu vinginevyo vilivyopigwa chapa na ambavyo ni miswada[1].

Na lengo langu kwenye ujumbe huu ni kumzindua Msunni anayehitaji kuzinduka ili asirubuniwe na taqiya ya Shia Imamiyah na maneno yao matamu wayasemayo kwenye minasaba ya kijamii na kwenye mikutano ya uhusiano na kwenye minasaba mingineyo, bali Masunni wanapaswa wawe na uelewa na weledi wa itikadi ya hawa jamaa na yaandikwayo ndani ya vitabu vyao.

Ni vyema wafuasi wa twariqa za Kisufi wakafahamu kuwa; Shia wanawalaghai wanapodai upendo, kuwaheshimu na kuwaiga Ahlil Bait, na kwamba upendo kama huo walionao wao ndio ule waliyo nao Shia, ili baada ya hapo wajione ni kama watu walio kwenye mrengo mmoja, na wanaopaswa kushirikiana dhidi ya waislamu wengine.

Yote haya ni sehemu ya kuficha ukweli (taqiya) unaohudumu maslahi yao katika kueneza Ushia, na hii ilitokana na mpango wa kilimwengu wa Shia unaolenga kuwaingiza Masunni kwenye Ushia, ulipokumbana na kikwazo cha wingi wa Masufi kwenye maeneo na nchi mbalimbali, na ikawa miongoni mwa wajibu wa kitaqiya ni kuwalaghai Masufi, kujipendekeza kwao na kuficha msimamo wao dhidi ya Masufi.

---

[1] Ar Risaalatu Al-ithnaa A'shariyah, uk 13, kwenye maelezo ya chini.

Na zitadhihiri kitabuni sababu mbalimbali za chuki halisi zilizowafanya Shia kuwahujumu Masufi na kuwakashifu, nazo si nyingine, ni ule mtazamo wa Masufi kuhusu Qur'an Tukufu, Sunna za Mtume, Swahaba na Mama wa Waumini, mtazamo huu wa Masufi ni mtazamo wa haki ambao unaenziwa na kila anayejinasibisha na Uislamu na Sunnah. Na msimamo huu ndio unaowafanya Shia wawe na uadui na vita.

Kwa uwezo wa Allah ujumbe huu utakuwa mfupi kwa kadiri iwezekanavyo, ambapo tutaja riwaya za Maimamu wa Shia Imamiyah jinsi wanavyowakufurisha, kuwapotoa na kuwaonya watu na Masufi, pasipo kuingilia au kutoa angalizo, bali tutamuacha msomaji ahukumu mwenyewe.

Na tutakapomtaja mwanazuoni yeyote wa Shia Imamiyah, mwisho tutaweka utambulisho wake, na tutaeleza jinsi alivyosifiwa na wanazuoni wa Shia Imamiyah, na kubainisha nafasi yake ya kielimu, ili kuepusha watu wasije kusema sisi tunanukuu kutoka kwa watu wasioeleweka, au isije kusemwa kwamba tunawasingizia Shia Imamiyah wasiyoyasema na wasiyoyaamini.

Na tutataja kwenye utangulizi wa kitabu dibaji fupi mno, ambapo tutataja baadhi ya itikadi za Shia Imamiyah ambazo zinatofautiana na itikadi za Masufi.

Allah Mtukufu tunamuomba awanusuru Masunni, na ajumuishe neno lao kwenye haki, na wafuate muongozo wa bwana wa Mitume, bwana wetu na kiigizo chetu Muhamad Nabii asiyejua kusoma kilichoandikwa, rehema na amani ya Allah iwe juu yake Yeye, jamaa zake na swahaba zake, na kila aliyefuata muongozo na mfumo wao mpaka siku ya kiyama.

***Umeandikwa na Abdallah ibn Mohammad***
***20/9/1435 Hijiria***

# MAKOSA YA KIITIKADI KATI YA MASUFI NA SHIA IMAMIYAH

Hizi ni itikadi za Shia Imamiyah ambazo zinakinzana na itikadi za Masufi, nayo ni misimamo asili ya kiitikadi na dini, na ambayo haipelekei kwenye uhusiano unaodaiwa, na wala haimfanyi mlinganiaji kulingania watu kwenye umoja kati ya Shia Imamiyah na Masufi.

**Msimamo wa Shia Imamiyah kuhusu Qur'an:**

**Kubadilishwa kwa Qur'an**[1]

Shia Imamiyah wanaamini hii Qur'an tuliyonayo imepotoshwa, na wakataja riwaya kadhaa zinazohusu hilo, kati yake:-

Kutoka kwa Hisham ibn Salim, naye kutoka kwa Abi Abdillah (amani ya Allah iwe juu yake): "Hakika Qur'an aliyokuja nayo Jibril (amani ya Allah iwe juu yake) kwa Muhammad (amani ya Allah iwe juu yake na jamaa zake) ina aya elfu kumi na saba"[2].

---

[1] Rejea Kitabu Usulu Madh-habus Shia'h Al-imamiyah Al-ithnaa Ashariyah (A'rdhu Wanaqd)" Cha Dr, Naswir Al-qiffaariy, 1/ 125-303.

[2] Usulul Kaafiy 2/634. Na riwaya hii imethibitishwa na Sheikh wao Al-majlisiy na akasema kwenye kitabu chake Mir-aatul U'qul 12/525: Na hadithi imethibitishwa. Kisha akasema: Hadithi ni sahihi, wala hakuna kificho kuwa; hadithi hii na hadithi nyingine sahihi zilizo wazi zinazoelezea upungufu na kubadilishwa kwa Qur'an, kwangu mimi hadithi hizi na za mlango huu maana yake ni Mutawaatir.

Ifahamike kuwa; idadi ya aya za Qur'an Tukufu ni aya (6236). Kwa maana hii Qur'an inayodaiwa na Raafidhwah (Shia) ni mara tatu zaidi ya Qur'an tuliyonayo - Qur'an ambayo Allah ameahidi kuilinda!!- Na Allah atukinge.

- Na Neematullahi Al-jazaairiy anasema: "Hadithi ni mashuhuri bali zimepokewa na wengi na zinafahamisha wazi kuwa Qur'an imebadilishwa kimaneno, mada na irabu"[1].

- Na Al-hurru Al-a'miliy anasema: "Jua, hakika haki ambayo hakuna kuikwepa kwa mujibu wa hadithi zilizopo, zifuatazo na nyinginezo kwamba; hii Qur'an tuliyonayo, ilikumbwa na mabadiliko fulani baada ya Mtume, na walioikusanya baada yake waliacha maneno na aya nyingi...!! Nami katika kuubainisha ukweli wa kauli hii baada ya kuzifuatilia hadithi na kuzichungua athari, ambapo twaweza kutoa uamuzi kuwa; hili ni katika mambo ya wajibu kwenye madhehebu ya Kishia"[2].

An Nuriy Attwabrasiy ametunga kitabu kinachothibitisha kubadilishwa kwa Qur-an na kukiita: (Faslul khitwaab fiy tahriyf Kitabi Rabbil Arbaabab), na ndani ya kitabu hiki ametoa maelezo mengi kuhusu kubadilishwa kwa Qur-an, na miongoni mwa dalili za kubadilishwa kwa Qur'an kwa upande wake ni:-

- Ufasaha wake wa hali ya juu kwenye baadhi ya vipengele ambavyo ni muujiza, na upuuzi (nonsense) kwenye baadhi yake, (yaani baadhi ya aya hazina maana - Allah atukinge)!! Na akainukuu Suratul "Wilayah" inayodaiwa na Shia kuwa; Sunna au swahaba ndio walioiondoa sura hii kwenye Kitabu cha Allah Mtukufu.

1 Al-anwarun Nu'maniyah 2/360-362

2 Mir-aatul An-waar uk 36

- Nayo ni: “Enyi mlioamini ziaminini nuru mbili tulizoziteremsha na zisomwazo kwenu na kuwaonyeni na adhabu kubwa, nuru mbili baadhi zipo kwa nyingine Nami ni mwenye kusikia na kujua, hakika wale wanaotekeleza (ahadi)na Mtume wake kwenye aya wana pepo zenye neema, na wale waliyokufuru baada ya kuamini kwa kuvunja ahadi yao na yale waliyoahidiwa na Mtume watarembewa motoni, wamezidhulumu nafsi zao na kumuasi wasii wa Mtume hao watanyweshwa maji ya moto[1].

- Pia wanasema: Ilisomwa kwa Abi Abdillahi:

﴿كُنتُمْ خَيْرَ أُمَّةٍ أُخْرِجَتْ لِلنَّاسِ﴾ [آل عمران: ١١٠]

- “Nyinyi ni uma bora mliyotolewa kwa watu”. Abu Abdillahi akasema: “Uma bora” utamuuwa Amiri wa waumini na Hasani na Husein (amani ya Allah iwe juu yao)!! Akasema: Basi nisomeje, Akasema: كُنتُمْ خَيْرَ أَئِمَّةٍ

- “Nyinyi ni Maimamu bora”[2].

- Na kadhalika anasema katika Suratul inshiraah: Kutoka kwa Abi Abdillah anasema: Hivi ndivyo ilivyoteremka: “Kwani hatukikunjua kifua chako. Na tukakuondolea mzigo wako. Uliovunja mgongo wako. Na tukatukuza utajo wako kwa Aliy mkwe wako”[3].

- Hizi ndio baadhi ya sura zilizopunguzwa zilizotajwa na An Nuriy Atwabrasiy, na akataja sura zote za Qur’an na upungufu uliyomo.

---

1 Faslul Khitaab uk 180

2 Faslul Khitaab uk 268

3 Faslul Khitaab uk 346

**Itikadi yao kuwa Qur'an si hoja mpaka kuwe na Qayyim**[1]

Haingii akilini kwa kundi lolote linalojigamba lenyewe kufuata uislam na kusema kuwa: "Qur'an sio hoja". Allah anasema kwa aliyetaka muujiza unaothibitisha ukweli wa Mtume:- (Je hayakuwatosha ya kwamba Tumekuteremshia Kitabu hiki wanachosomewa?)[2] Qur'an Tukufu ndio shahidi na hoja.

Lakini Sheikh wa Kishia na ambaye humuita "Thiqatul Islam" (Al-kulayniy) anapokea kwenye kitabu chake "Usulul Kaafiy" kama inavyosomeka: "...Kuwa Qur'an haiwezi ikawa hoja mpaka kwa Qayyim: na Aliy ndio alikuwa Qayyim wa Qur'an, na kumtii ni faradhi, na (Aliy) alikuwa hoja kwa watu baada ya Mtume"[3]

Na maana ya maneno haya ni kuwa kauli ya Imamu ni fasaha zaidi kuliko maneno ya Allah, na kwa hivyo ndipo wakakiita Kitabu cha Allah ni Qur'an iliyo kimya, na wakamwita Imamu kuwa ni Qur'an inayonena. Na wanapokea kutoka kwa Aliy kuwa alisema: "Hiki ni kitabu cha Allah kilicho kimya, Nami ni Kitabu kinachonena"[4].

Na kuna wakati mwingine hudai kuwa Maimamu ndio Qur'an yenyewe, na hulifasiri neno la Allah Mtukufu: (...Na kuifuata nuru iliyoteremshwa pamoja naye...)[5] Na ndio ukawa-

---

1 Mustafaad min Kitabi "Usulu madh-habis Shia'til imamiyah AL-ithnaa Ashariyah 1/127-132.

2 Qur'an 29:51

3 Usulul Kaafiy 1/188

4 Al-hurru Al-a'miliy - Al-fusulul Muhimmah uk 235

5 Qur'an 7:157

kuta wanalifasiri neno la Allah: An Nur kuwa ni: Aliy na Maimamu ()[1].

**Itikadi ya Shia kuwa Maimam wana upekee wa kuijua Qur'an hawana ushirika na yeyote.**

Imekuja hadithi ndefu kwenye Usulul kaafiy kutoka kwa Abi Abdillahi akisema: "Hakika Qur'an inawatosha watu lau watampata wakuifasiri, na Mtume (amani ya Allah iwe juu yake) alishaifasiri kwa mtu mmoja, na kuifasiri kwa uma ni suala la yule mtu - naye ni Aliy ibn Abi Twalib"[2]

Na kutoka kwa Abi Jaa'far:..."Si kingine kwa watu isipokuwa waisome Qur'an kama ilivyoteremshwa, na iwapo watahitaji tafsiri yake, basi muongozo tunao na wakufuatwa ni sisi[3]"

**Neno lao, sehemu kubwa ya Qur'an imeteremka kwao na kwa maadui wao:**

Shia wanasema wakinukuu kutoka kwa Maimamu wao kuwa: "Sehemu kubwa ya Qur'an imeteremka kwao (yaani kwa Maimamu Ithnaa Asher) na kwa wapenzi wao na maadui zao[4]"

Pamoja na hivyo kama utafanya upembuzi kwenye Kitabu cha Allah, na ukachukua Kamusi zote za lugha ya Kiarabu na ukatafuta jina miongoni mwa majina ya hawa Maimamu wa Ithnaa Asher katu hutokuta utajo wao!!

Lakini pamoja na hivyo, Sheikh wao Al-baharaniy anadai

---

1 Al-kaafiy 1/194

2 Usulul Kaafiy 1/25, na Wasaailus Shia'h 18/131

3 Wasaailus Shia'ah cha Al-a'miliy 27/202

4 Tafsiyrus Swaafiy 1/24

Aliy pekee ametajwa ndani ya Qur'an mara (1154), na katika mnasaba huu ametunga Kitabu na kukiita "Allawaami'un Nuraaniyatu fiy Asmaai Aliy Wa Ahli Baytihi Al-Qur'aniyah"

Muandishi ndani ya kitabu hicho amevunja viwango vya lugha ya Waarabu, na kuikiuka misingi ya akili na mantiki.

Na zimekuja baadhi ya riwaya zao zinaeleza: "Qur'an iliteremka robo nne: robo moja kwetu sisi, na robo kwa maadui wetu, na robo ni sunan na mafumbo, na robo ni faradhi na hukumu mbalimbali"[1]

Na katika riwaya kutoka kwa Amirul Muuminina (amani ya Allah iwe juu yake) "Qur'an iliteremka robo nne: robo moja kwetu sisi, na robo kwa maadui wetu, na robo ni sunan na amthaali, na robo ni faradhi na hukumu mbalimbali, na ile yenyewe ipo kwetu[2]"

Na katika riwaya nyingine kutoka kwa Amirul Muuminina (amani ya Allah iwe juu yake): "Qur'an iliteremka robo tatu, theluthi kwetu, na (theluthi) kwa adui yetu, na theluthi ni sunan na amthaali, na theluthi ni faradhi na hukumu mbalimbali[3]

[1] Usulul Kaafiy 2/627, na Al-burhaan: 1/21

[2] Bihaarul An-waar 24/306

[3] Usulul Kaafiy 2/628

## Msimamo wa Shia Al-imamiyah kuhusu sunna za Mtume

Sunna za Mtume zinachkuliwa kuwa ni chanzo cha pili cha kisharia baada ya Qur'an Tukufu, nazo ni sehemu ya wahyi wa Allah aliyomhusisha nao Mtume (amani ya Allah iwe juu yake), Mtume wa Allah hazungumzi kwa utashi, na kwa hivyo kutii, kunyenyekea na kusalimu amri kwenye madhumuni ya sunna ndio muktadha wa kushuhudia kuwa Mohammad ni Mjumbe wa Allah (amani ya Allah iwe juu yake), Mjumbe kutoka kwa Mfalme wa walimwengu wote, na ndiye aliye na jukumu la kuifikisha dini kwa watu wote.

Allah anasema: (Basi wajihadhari wale wanaokaidi amri Yake, Usije ukawapata msiba au ikawafika adhabu iumizayo)[1] Na pia amesema: (Naapa kwa (haki ya) Mola wako, Wao hawawi wenye kuamini (Kweli kweli) mpaka wakufanye (wewe ndiye) hakimu (mwamuzi) katika yale wanayokhitilafiana, kisha wasione uzito nyoyoni mwao juu ya hukumu uliyotoa, na wanyenyekee kabisa)[2]

Na Mtume (amani ya Allah iwe juu yake) anasema: "Nisimkute kabisa mmoja wenu ameketi kwenye kiti chake,

---

[1] Qur'an 24: 63

[2] Qur'an 4: 65

yamjia hadithi miongoni mwa hadithi zangu, katika yale niliyoyaamrisha au kuyakataza, akasema: Sisi hatujui. Kile tulichokuta kwenye Kitabu cha Allah tunakifuata".[1]

Na Imam Shafi'iyu (Allah amrehemu) anasema: "Sijamsikia yeyote aliyenasibishwa na watu au aliyejinasibisha mwenyewe kwenye elimu akakhalifu kuwa Allah Mtukufu amefaradhisha kufuata amri ya Mtume (amani ya Allah iwe juu yake) na kusalimu amri kwenye hukumu yake, kwani Allah Mtukufu hakumjaalia yeyote baada yake isipokuwa kumfuata, na kwamba hailazimu kauli katika mazingira yoyote isipokuwa kwa kauli ya Allah au sunna ya Mtume wa Allah (amani ya Allah iwe juu yake), na kwamba kilicho kinyume na viwili hivyo kinatakiwa kufuata viwili hivyo, na kwamba faradhi ya Allah kwetu na kwa waliyo kabla yetu na baada yetu ni kuzikubali hadithi kutoka kwa Mtume na hakuna mjadala kuwa ni wajibu kukubali hadithi kutoka kwa Mtume ﷺ"[2].

Ama Shia wameziacha sunna nyuma ya migongo yao, na hawakuipa uzito wowote amri ya Allah inayotutaka kumfuata Mtume, na wakaja na maana ya sunna isiyotoka kwa Allah na wala haijapata kufikiriwa na waliyotangulia.

Sunna kwa Shia ni: "Ni kila kitokacho kwa asiye na makosa miongoni mwa kauli, au kitendo au kuona jambo na kulinyamazia"[3].

Na waliyohifadhiwa na makosa kwa Shia, ni Mtume (amani ya Allah iwe juu yake) na Maimamu wao kumi na mbili.

---

1 Imepotolewa na Abu Daud, Tirmidhiy na Ibn Majah

2 Al-ummu 7/287

3 Mohammad Taqiyyu Al-hakiym - Al-usul a'mmah lilfiqhil Muqaran uk 122

Na hivi ndivyo Maimamu wao wanavyopata haki ya kutiiwa na wajibu wa kufuatwa kama Mtume wetu (amani ya Allah iwe juu yake), hakuna tofauti kati ya Maimamu na yule asiyezungumza kwa utashi, isipokuwa wahyi utakao kwa Allah.

Na kwa msingi huo ndio mmoja wa Masheikh wao wa zama hizi Abdallah Al-fayyadh anasema: "Hakika suala la kuamini kutokosea kwa Maimamu, ni kuyafanya mazungumzo yatokayo kwao ni sahihi pasipo kushurutisha isnadi (mlolongo) wake kufika kwa Mtume kama ilivyo kwa Ahlus Sunnah"[1], Na sababu yake ni kuwa, Uimam kwa Shia ni "Muendelezo wa Utume". Kama asemavyo Sheikh wao Muhammad Ridhwaa Al-mudhwaffar[2]

Na ibn Baabawayhi Al-qummiy amechukua msimamo wa Maimamu ni kama Mitume: "Kauli yao ni kauli ya Allah, na amri yao ni amri ya Allah, kuwatii ni kumtii Allah, na kuwaasi ni kumuasi Allah, na wao hawatamki isipokuwa kwa niaba ya Allah na ni wahyi wake"[3].

Na kwa dhamira ya kuiuza itikadi hii, Shia wamesema uongo kupitia ndimi za maimamu wao kuwa wao ndio waliyoamrishwa hayo, Imekuja kwenye kitabu Al-kaafiy kutoka kwa Abi Abdillahi akisema: "Simulizi yangu ni simulizi ya baba yangu, na simulizi ya baba yangu ni simulizi ya babu yangu, na simulizi ya babu yangu ni simulizi ya babu yangu Husein, na simulizi ya Husein ni simulizi ya Hasan, na simulizi ya Hasan ni simulizi ya Amirul Muuminina, na simulizi ya Amirul Muuminina ni

[1] Abdullahi Fayyadh - Taarekhul Imamah uk 140

[2] Mohammad Ridhwaa Al-mudhwafaar - Aqaaidul Imamiyah uk 166

[3] Ibn Baabawayhi - Al-I'tiqadaat uk 106

simulizi ya Mtume wa Allah, na simulizi ya Mtume wa Allah ni kauli ya Allah Mtukufu[1]"

Na mshereheshaji wa Al-kaafiy ameeleza kwamba kauli hii inajuilisha kuwa; "Hadithi ya Imamu yeyote Mtwaharifu ni kauli ya Allah Mtukufu, wala hakuna mgongano kwenye kauli zao, kama ambavyo hakuna mgongano kwenye neno la Allah Mtukufu[2]"

Na tunaporejea kwenye vitabu vya shia vya itikadi na fiqh, tunakuta wanaikiuka itikadi hii potofu - yaani Maimamu kushirikiana na Mtume ﷺ katika kufikisha na kutiiwa, tutakuta shia wamewapa Maimamu wao hadhi sawa na Mtume ﷺ, na katu hatukuti amri na makatazo ya Mtume ﷺ isipokuwa idadi chache mno tena kwa kuona haya, wakati huo huo hadithi za Maimamu wao zinazidi maelefu...Hivi kweli shia wanaamini kama Muhammad ni Mjumbe wa Allah! Hasha wakala..

---

1 Usulul Kaafiy, Kitabu Fadhlul ilmi, Baabu Riwayatul Kutub Wal-hadiyth: 1/53, Wasaailus Shi'ah: 18/58

2 Al-mazindraniy - Sher-hu Jaami'u (A'lal kaafiy) 2/272

# MSIMAMO WA SHIA IMAMIYAH KUHUSU SWAHABA WA MTUME

Swahaba watukufu wa Mtume ni watu wenye hadhi na heshima kubwa kwa waislamu, swahaba ni viumbe bora baada ya Mitume, ni watu wenye nafsi na nyoyo safi. Allah amewateua kusuhubiana na Mtume wa mwisho wa Mola wa viumbe wote ﷺ, na ni vigumu kuja baada yao watu bora kuliko wao.

Na hii ni kwa ushahidi wa bwana wa viumbe Mtume wetu Muhammad ﷺ, ambapo alisema: "Watu bora ni wa karne yangu kisha wanaowafuatia kisha wanaowafuatia"[1].

Na kwa nini isiwe hivyo wakati Allah amewatakasa toka kwenye mbingu saba - Allah Mtukufu anasema: (Na wale waliotangulia wakawa wa kwanza miongoni mwa Muhajirina na Answari, na wale waliowafuata kwa mwendo mzuri Allah amewaridhia nao wakamridhia na amewaandalia Mabutsani yapitayo mito mbele yake, watakaa humo milele. Huku ndio kufuzu kukubwa)[2]

Na Allah anasema: (Muhammad ni Mtume wa Allah. Na walio pamoja naye ni wenye nyoyo thabiti mbele ya makafiri na wenye kuhurumiana wao kwa wao. Utawaona wakiinama kwa kurukuu na kusujudu, wakitafuta fadhila za Allah na radhi yake.

---

1 Al-bukhariy Namba: (2652), na Sahihul Muslim Namba: (2533)

2 Qur'an 9:100

Alama zao zi katika nyuso zao, kwa athari ya kusujudu. Huu ndio mfano wao katika Taurati. Na mfano wao katika Injili (wametajwa hivi): Kuwa ni kama mmea uliotoa matawi yake; na (matawi) yakautia nguvu; ukawa mnene ukasimama sawasawa juu kigogo chake, ukawafurahisha walioupanda; ili awakasirishe makafiri kwa ajili yao. Allah amewaahidi walioamini na kutenda mema katika wao msamaha na ujira mkubwa)[1]

Na Allah anasema: (Kwa hakika Allah amewaridhia waislamu waliofungamana nawe chini ya mti; na alijua yaliyomo nyoyoni mwao. Basi akateremsha utulivu juu yao, na akawapa kushinda kwa zama za karibu)[2]

Na Imam Attwahawiy anasema: "Na twawapenda swahaba wa Mtume wa Allah, wala hatuchupi mpaka kwenye upendo wa yeyote kati yao, na wala hatujitengi na yeyote kati yao, na tunamchukia anayewachukia na kuwataja vibaya, wala hatuwataji isipokuwa kwa wema, na kuwapenda swahaba ni dini, imani na ihsani, na kuwachukia ni kufuru, unafiki na kuchupa mpaka.

Ama itikadi ya Raafidhwah imejikita katika kuwatukana, kuwashutumu na kuwakufurisha swahaba (Allah awaridhie), na kumkufurisha kila anayewapenda swahaba.

Imekuja kwenye kitabu cha Al-kaafiy: Kutoka kwa Hannan, naye kutoka kwa baba yake, naye kutoka kwa Abi Ja'far (amani ya Allah iwe juu yake) "Watu (wote) waliritadi baada ya Mtume isipokuwa watatu, nikasema: Ni wepi hao watatu? Akasema: Ni Miqdadi ibn Al-as-wad, Abu Dhari Al-ghifariy, na Salmani Al-farisiy"[3]

---

1 Qur'an 48: 29

2 Qur'an 48: 18

3 Al-kaafiy: 8/245

Na Al-majlisiy ametaja kwenye (Biharul An-waar): Kwamba mtwana wa Ali ibn Al-husein alisema: Nilikuwa na (Ali ibn Al-husein) kwenye baadhi ya faragha zake, nikasema: "Mimi nina haki kwako (lazima) uniambie kuhusu hawa watu wawili: Kuhusu Abi bakri na Omar? Akasema: Wote wawili ni makafiri, na anayewapenda ni kafiri". Na kutoka kwa Abi Hamzah Atthamaaliy kuwa Yeye alimuuliza Aliy ibn Al-husein kuhusu wawili hao (Abi bakri na Omar) Akasema: "Wote wawili ni makafiri na anayewapenda ni kafiri"[1]

Na katika tafsiri ya Al-qummiy kwenye neno la Allah: (...na anakataza uchafu na uovu, na dhulma)[2] Wamesema: "Uchafu ni Abu Bakri, uovu ni Omar na dhulma ni Othmani"[3]

Na Al-majlisiy anasema kwenye (Biharul An-waar): "Hadithi zinazoeleza ukafiri wa Abi Bakri na Omar na mfano wao, na thawabu za kuwalaani na kujiepusha nao, na kujumuisha uzushi wao, ni nyingi mno haziwezi kutajwa zote kwenye juzuu hii au juzuu nyinginezo, na tuliyoyataja yanakidhi haja kwa mtu Allah anayetaka kumuongoza kwenye njia iliyo nyooka"[4]

Bali Al-majlisiy ametaja kwenye (Biharul An-waar): riwaya kadhaa kuwa Abi Bakri, Omar, Othmani na Mua'wiyah wote wapo kwenye masanduku ya moto - Allah atukinge!

Na si hivyo tu, wamefanya maeneo ya kukidhia haja ndio maeneo matukufu zaidi katika kuwalaani swahaba (Allah awaridhie), Attuusiyrkaniy ambaye huitwa Meya wa wanazuoni

---

1 Bihaarul An-waar, cha Al-majlasiy 69/137-138

2 Qur'an 16: 90

3 Tafsiri Al-qummiy 1/390

4 Bihaarul An-waar 30/399

na wahakiki anasema: “Jua, kuwa sehemu tukufu zaidi, wakati bora na mazingira mnasaba kuliko yote ya kuwalaani -laana iwashukie- ni pale unapokuwa chooni, sema kwa kurudia rudia kwa kujitakasa na kila mmoja: Ewe Mola mlaani Omar, Abu Bakri na Omar, kisha Othman na Omar, kisha Muawiyah na Omar, kisha Yazid na Omar, kisha Ibn Ziyad na Omar, kisha Ibn Sa’ad na Omar, halafu Shimri na Omar, kisha askari wao na Omar. Ewe Mola mlaani Aisha na Hafsa na Hindu na Umul Hakam, na umlaani kila anayeridhia vitendo vyao mpaka siku ya kiyama”[1]

Maelezo haya yanaonesha chuki yao iliyojificha kwa masahaba watukufu, ambapo wameyafanya maeneo machafu kuwa ndio maeneo matukufu zaidi ya kuwalaani swahaba, na wakaufanya wakati wa kukidhi haja ndio wakati bora zaidi wa kulaani.

Hivi, ipo dini miongoni mwa dini zilizopo inayowaamuru watu wake kuwatukana wafu na kuburudika kwa kuwalaani wafu mpaka kwenye wakati wa kukidhi haja!!

[1] Laaliy AL-akhbaar 4/92

# MSIMAMO WAO KWA MAMA WA WAUMINI

Itikadi ya shia imejikita juu ya kuwachukia na kuwafanyia uadui Mama wa waumini (Allah awaridhie), na hasa Aisha bint Abi Bakri (Allah amridhie na baba yake Asswidiq), na Hafsa bint Omar ibn Al-khattwab (Allah amridhie na baba yake Al-farouq).

Sheikh wao Al-majlisiy anasema: "Na itikadi yetu kuhusu kujitenga, sisi tunajitenga na masanamu manne Abi Bakri, Omar, Othman na Muawiyah, na katika wanawake kuna wanne Aisha, Hafswa, Hindu na Umul Hakam na wafuasi na watetezi wao wote, na kwamba wao ni viumbe waovu wa Allah waliyo ardhini, na kwamba haitimii imani ya kumuamini Allah na Mtume wake na Maimamu isipokuwa baada ya kujitenga na maadui wao"[1]

Na miongoni mwa chuki zao zilizojificha kwa Mama wa waumini, ni kumtuhumu kwao Aisha na Hafswa kuwa ndio waliyomuua Mtume (rehema na amani ya Allah iwe juu yake), Al-'ayyash amepokea kwa sanad (mlolongo) mpaka kwa Abi Abdillahi Ja'far Asswadiq kuwa alisema: "Mwajua Mtume ﷺ, na jamaa zake alikufa au aliuliwa?

Allah anasema: (Akifa au akiuawa ndio mtarudi nyuma,

[1] Haaqul Yaqin, cha Mohammad Al-baaqir Al-majlisiy uk 519

muwe makafiri kama zamani?)[1] Alipewa sumu kabla ya kufa; Wawili hao[2] walimnywisha sumu kabla ya kufa. Na tukasema: Wawili hao na baba zao ni miongoni mwa viumbe waovu wa Allah[3].

Na Al-majlisiy ameielezea sanad ya riwaya hii kuwa ni yenye kuzingatiwa, na akaitolea maelezo kwa neno lake: "Hakika Al-'ayyashiy amepokea kwa sanad inayozingatiwa kutoka kwa Asswadiq (amani iwe juu yake) kuwa Aisha na Hafswa laana ya Allah iwashukie wao na baba zao ndio waliyomuua Mtume wa Allah kwa sumu waliyoipanga wawili hao"[4]

Na miongoni mwa chuki zao kwa Aisha na Hafwa (Allah awaridhie), ni dai lao kuwa; Allah alipiga mfano wa mke wa Nuhu na mke wa Luti kuwapigia Aisha na Hafswa (Allah awaridhie) (Allah amewapigia mfano waliokufuru: mke wa Nuhu na mke wa Luti. Walikuwa chini ya waja wetu wema wawili miongoni mwa waja wetu. Lakini wakawakhini waume zao, nao wasiwafae kitu. Na ikasemwa: Ingieni Motoni pamoja na wanaoingia!)[5] Sheikh wao Al-faydhul Kaashaniy kwenye tafsiri yake: Allah alipiga mfano wa hali za makafiri na wanafiki kwamba wataadhibiwa kwa kufuru na unafiki wao wala hautozingatiwa ukaribu wao na kuungana kwao na Mtume ﷺ kwa hali yoyote kama ilivyokua kwa mke wa mke wa Nuuh na

1 Qur'an 5:144

2 Al-kaashaniy akaongeza: (Yaani Allah awalaani wanawake wawili hao na baba zao) Tafsiri Asswaafiy 1/305

3 Al-kaashaniy 1/305, Al-burhani cha Al-bahraaniy 1/320, na Bihaarul An-waar cha Al-majlisiy 6/504, 8/6

4 Hayaatul Qulub cha Al-majlisiy 2/700

5 Qur'an:10

mke wa Luut. Na hapa pana fumbo kwa Aisha na Hafsa kwa khiana waliomfanyia Mtume ﷺ na kumfanyia unafiki na kumpinga kama walivyofanya wake wa Mitume hao,wakawa hawakuwasaidia kitu).

Al-majlisiy anasema wakati anaielezea aya hii: "Wala hakuna siri kwa mkosoaji makini na mwerevu mwenye busara kuhusu ishara ya aya bali uwazi kuhusu unafiki wa Aisha na Hafsa na kufuru zao"[1]

Kama ambavyo haikusalimika heshima ya Mama wa waumini aliye twahara na kutwaharishwa, na ambaye alitakaswa na Allah kutoka kwenye mbingu saba, (Raafidhwah) walimtuhumu uchafu -Allah atukinge- bila shaka huku ni kumkadhibisha Allah ambaye aliteremsha aya za kumtakasa na ambazo zinasomwa mpaka siku ya kiyama, na huku ni kumtusi Mtume (amani ya Allah iwe juu yake).

Na Rajab Al-barsiy anaeleza kuwa: "Aisha alikusanya dinari arobaini zitokanazo na khiyana na kuzigawanya kwa wanaomchukia Aliy[2]".

Bali wakamfanya mke wa Mtume (amani ya Allah iwe juu yake) ni mhamasishaji wa uzinzi na ukahaba, Attwabrasiy ametaja kwenye kitabu chake Al-ihtijaj: "Kwamba kuna siku Aisha alimpamba msichana aliyekuwa kwake, na akasema: huwenda tukamnasa kijana miongoni mwa vijana wa Kiquraysh atayepagawishwa naye"[3].

---

1 Bihaarul An-waar 22/33

2 Mashaariq An-waaril Yaqin" cha Rajab l-barsiy uk 86

3 Al-ihtijaaj uk 82

# DUA YA MASANAMU MAWILI YA KIQURAYSH

Wanachokusudia ni kumuapiza Abu Bakri, Omar, Aisha na Hafsa (Allah awaridhie).

Imekuja ndani yake: Kwa jina la Allah mwingi wa rehema mwenye kurehemu,, Ewe Mola mrehemu Mohammad na jamaa wa Mohammad, Ewe Mola yalaani masanamu mawili ya Kiquraysh na mataghuti yao na waongo wao na watoto wao, walokhalifu amri zako na wakapinga wahyi wako, na wakakanusha neema zako, na wakabadili dini yako, na wakapotosha kitabu chako, ewe Mola walaani wao na wafuasi wao, mawalii wao, na makundi yao, ewe Mola walaani ndani ya siri zao na Dhahiri yao, laana iliyo kubwa ya daima," mpaka akafikia kusema katika dua yake hii ndefu, na akakariri mara nne, ewe Mola waadhibu adhabu ambayo mpaka watu wa motoni watawaombea msaada. [1]

Kama ambavyo hushereheka kwenye siku aliyouawa Al-farouq Omar ibn Al-khatwab na humwita aliyemuua Omar Abu Lu-uluatul Majuusiy: Baba shujaaddin.[2]"

---

1 Ihqaaq alhaq wa izhaa albatil uk 138

2 Abas Al-qummiy, (Alkunaa Wal-alqaab 2/55)

# MSIMAMO WA SHIA AL-IMAMIYA AL-ITHNAA'SHARIYAH KWA MASUFI

**Masufi mbele ya Shia Al-imamiya ni watu waovu, waliyolaaniwa na kufukuzwa kwenye rehema za Allah.**

Al-amiliy[1] anasema kwenye utangulizi wa kitabu chake: ''Nilipoona miongoni mwa Shia wengi dhaifu wameacha njia ya wakongwe na Maimamu wao kwenye hukumu za sheria, na kufuata nyendo za maadui wao ambao hawataki kabisa kurudi kwa Maimamu (amani iwe juu yao) kwenye hukumu za dini, na badala yake wakazusha msamiati wao wenyewe wa kidini na kujiita Masufi wala hawakujinasibu na Mtume na Maimamu, ambao ndio viumbe bora, hilo likapelekea hawa madhaifu kuafiki itikadi na matendo ya waovu hao na kuwafuata, kwa vile walikuwa wanawalaghai watu kwa kudhihirisha uchamungu na kuonyesha uzuhudi kama vile walivyofanya maimamu (Allah awarehemu) Na hiyo kwako na iwe ni dalili tosha ya upotofu wa njia zao.[2]

---

1 Abuu Ja'afar Muhamad ibn Sheikh Al-hasan ibn Ali Al-huru Al-amiliy ndio mwenye Kitabu ''Wasaailus Shia'' moja ya vitabu vinane vya Shia Al-ithnaa Ashariya. Sheikh Yusuf Al-baharniy anamuelezea: Alikuwa mwanazuoni mtukufu, mtaalamu wa hadithi na historia'', Lu-uluatul Bahrayn uk 76, Tarjamah Namba 28. Na Al-khonsaniy anasema: ''Sheikh wetu Al-hurru Al-amiliy ni mwana historia, na ndiye mwenye kitabu Wassailus Shia, na ni mmoja wa Muhamad watatu wa mwisho waliyoikusanya sheria hii''. Rawdhwaatul Jannaat 7/96, Tarjama Namba 605.

2 Rejea Kitabu Ar Risalatu Al-ithnaa'shariya fir Radi A'laa Suufiyah uk 3.

Na Shia Imamiya wamepokea hadithi nyingi zinazotahadharisha kuwa na uhusiano na michanganyiko na Masufi, kwani Masufi ndio chanzo cha ushetani na kuwapoteza watu, Masufi wanajifanya kudhihirisha ufukara na kuipa nyongo dunia kwa lengo la kuwaghilibu wapumbavu na kuwadanganya wajinga.

Mhakiki wao huyu wa zama hizi Al-mirza Habibullah Alhashimiy Al-khoiy anataja riwaya katika kuwalaani Masufi, na anadai kuwa; Masufi wamefukuzwa kwenye rehema za Allah, Anasema: "Kwa hakika imekubainikia na kukuthibitikia waliyoyaeleza katika ufafanuzi wa haya maneno ya Amiri wa Waumini (amani iwe juu yake) kuwa Madhehebu ya Kisufi kwa ujumla wake yanakwenda kinyume na madhehebu ya kisheria Imaamiyya ambayo ndio ya haki na ya kisheria, Allah aimarishe jengo la madhehebu haya na nguzo zake na misingi yake.... kama ambavyo pia imeshakubainikia kuwa aya na hadithi zinazowalaani, kuwakosoa, kuwasema kwa mafumbo, na kuwadharau ni nyingi sana. Na riwaya walizoshikamana nazo kundi hili la kizushi, lililofukuzwa na kulaaniwa, imani za uongo...au zenye tafsiri tata, au dhaifu..., Ole wao watu waliowafanya watangulizi wao waliowawekea uzushi na kuwaghilibu kwa mambo ya upotovu kuwafanya ni miungu, na wakaridhika na Shibliy, Ghazaaliy, Ibn Arabiy na Al-juneyd na kuwafanya ni Maimamu, Allah awalaani duniani, na awaongezee adhabu akhera"[1]

Na mwanazuoni wao wa kishia Alhuru Al aamily ameweka mlangao kamili katika kitabu chake (Arrisaala al ithnaashiriya fii rradi alaa ssuufiyya), na ametaja riwaya kadhaa na kauli mbali mbali katika mlango huo ambazo zinawataja vibaya masufi na zinawajibisha kuwalaani na kujitenga nao. Na miongoni mwa

[1] Angalia Kitabu- Minhaajul Bara'h fi Sharhi Nahjil Balagha 14/21

aliyoyasema ni: " Wamesema baadhi ya mashekh wetu wachambuzi wa kisasa: Tambua kwamba jina hili la kisufi lilikuwa linatumika kwa kikundi cha hukamaai walioacha njia sahihi,kisha jina hili likatumika kwa kundi la wazandiki waliokwenda kinyume na wakawa maadui wa aali Muhammad ﷺ kwa mfano Alhasan Albasry, Sufiyaan Athauriyy na mfano wao, kisha likaja kutumika kwa waliokuja baada yao na wakafata njia yao kama vile Alghazaaly ambae anaongoza uadui dhidi ya Ahlil Bait. Wala hakuna shia wa Imaamiyya aliyetumia jina hilo si katika zama za Maimamu wala zama zilizofuatia[1].

[1] Angalia kitabu - Arrisaala al ithna ashiriyyah fii rradi alaa ssuufiyya uk.15

## MASUFI MBELE YA MASHIA NI MAYAHUDI WA UMMA HUU NA NI WAPOTOFU KULIKO MAKAFIRI NAO NI WATU WA MOTONI NA AMALI ZAO NI AMALI ZA WATU WAOVU

Amenukuu Alhuru al-amiliy katika kitabu chake "al-risala al-ithna asheriya fiy rradi ala sufiya" kutoka kwa sheikh wake Bahaudin Muhammad al-amily katika kitabu chake al-kashkuul, kasema, amesema Mtume ﷺ "Hakitasimama kiyama mpaka watakuja watu katika umma wangu wanaitwa masufi, sio katika watu wangu, bali ni mayahudi wa umma huu nao ni wapotovu kuliko makafiri, nao ni watu wa motoni, wanaume wananyoa nywele, na wananyanyua sauti zao kwenye dhikri, na wanadhania kwamba wamo kwenye njia ya watu wema, lakini kumbe wao ni wapotovu kuliko makafiri, nao ni watu wa motoni sauti zao ni kama milio ya punda, mpaka akasema na matendo yao ni matendo ya watu waovu.[1]

Baadae akatia sherhe Al-hur Al-amily katika hadithi hii na nyengine na dalili nyengine alizozitoa katika kuwatukana masufi akasema, "Nasema atakaeangalia kauli zilizotangulia na zinazofuata atafahamu kwamba mambo muhimu ya dini hayakucham-

[1] Tazama risala Al-itna ashiriya fiy arradi ala asufiya, uk16. Na Alfusulu muhima

buliwa na kutajwa kwa uwazi hadi kufikia upeo huu na hii ni kwa muktadha wa sharia kwani walitambua kwamba fitina hii ni katika fitina kubwa za dini, ni shubha yenye nguvu kwa madhaifu wa al-imamiyah, kwani waliotangulia na waliokuja mwisho katika masufi bado ni wenye kuwaghururi watu na kuwahadaa kwa kudhihirisha uzuhudi, unyenyekevu na ibada waonyeshe kwamba hizo ni sababu za mafanikio, na baadae katikati wanawapambia na kutia bidaa ambazo zinawatowa katika dini, na kuwapoteza dhidi ya njia iliyonyooka kama vile kuwatoa kwenye itikadi ya Alhuluul na al-itihadi (kuchanganyika na kuyeyuka), na mengine hata kufikia kupelekea al-itna asheriya kugawika sehemu mbili, kila mmoja akawa ni mwenye kumpotosha mwenzake, wakawa wafuasi wengine ni wenye kukaa na viongozi wao na wanakubali kauli zao na wengine wanatolewa katika dini kwa ukamilifu, Allah atuepushe na mtihani huu.

Na anasisitiza Alhur Al-aamily tawaturi ya hadithi zenye dalili ya kuwakosoa masufi na kuwalani na kuwahukumia kuwa ni makafiri na kuwa ni wazandiki, kwa kukusanya ndani ya kitabu chake "Al-ithna asheriya fiy arradi ala sufiya, " hadithi zaidi ya elfu kutoka kwa Mtume ﷺ na maimamu dhidi ya masufi na kuwalaani na kubatilisha kila jambo lao.

# MSIMAMO WA MAIMAMU WA KISHIA KWA MASUFI

**Imam Al-saadiq anatoa hukumu kwamba masufi ni maadui wa ahlu albayt na anaewarudi ni sawa na mujahidin mbele ya Mtume ﷺ**

Amesema Muhadithi wa kishia Abbas Alqumiy kwenye kitabu chake "safiynat al-bihar, kutoka kwa Abu Abdillah Al-saadiq, kwamba mtu mmoja alimuuliza kuhusu watu watakaodhihiri katika zama hizi, wanaitwa masufi? akasema " Hao ni maadui wetu, atakaewafuata atakuwa ni mmoja wao na atafufuliwa pamoja nao, na kutakuwa na watu watakaodai kutupenda, watawafuata watu hao na wanajishabihisha nao na watajiita kwa majina yao na wataeneza kauli zao, atakaewafuata hatakuwa nasi nami nitakuwa mbali nae, na atakaewakataa na kuwarudi atakuwa ni sawa na aliepigana jihadi pamoja na Mtume wa Allah[1].

[1] Safiyna al-bihary cha almuhadithi alqumiy uk 5664

# MSIMAMO WA IMAMU AL-SADIQ JUU YA MASUFI NA HUKUMU KWAMBA NI WATU WA ITIKADI MBOVU

Amesema Al-ardabily katika kitabu chake ''Hadiyqatu asshiya'', kutoka kwa Imam Abu Muhammad Alhassan al-skariy, kwamba amesema, aliulizwa Abu Abdillah Al-saadiq, kuhusu hali ya Abu hisham Alkufiy akasema '' Alikuwa na akida mbovu kabisa, nae ndiye aliyezua madhehebu yanayoitwa tasawuf na akaifanya ndio makao yake ya itikadi yake potofu, na katika vitabu vyengine (makao ya nafsi yake khabithi)

# MSIMAMO WA IMAMU MUSSA BIN JAAFAR KWA TASAWUF

Amesema Seyyid Hashim Al-bahraaniy katika kitabu chake ''Hilyat al-abraar'', kutoka kwa Shaqiiq Al-balkhiy ''Nilihiji nikamuona mtu mmoja mweusi amekaa peke yake, nikasema ndani ya nafsi yangu, huyu ni mtu wa tasawuf anataka kuwa mzigo kwa wenzake'' akanitazama na kusema ''ewe Shaqiiq ''Jiepushe na dhana nyingi hakika baadhi ya dhana ni dhambi'', nikajuta na kusema ''Hakika huyu ni mja mwema amenitaja kwa jina langu, akayasema yaliyo ndani ya nafsi yangu bila ya mimi kuyatamka, nitamtaka radhi nitakapomuona, na aliponiona mara ya pili akasema, ''Ewe Shaiqiq ''Na mimi ni msamehevu kwa mwenye kuamini na akafanya amali njema na akaongoka '' Na alipofika Makka nikamuulizia nikaambiwa huyo ni Mussa bin Jaafar[1]

Al-hur Al-amily amesherehesha riwaya hii na akasema;

Tazama namna alivyomkemea yule aliemnasibisha na tasawuf ambayo haikuja katika sharia, na jinsi alivyomkataza jambo hilo na kumuamrisha ajiepushe na tuhuma hii, wala hakuridhika kuitwa kwa jina hili, ama alipoitwa kwa hali nzuri yenye kuwafikiana na maandiko ya kisharia, na kumpa jina hili

[1] Hilyatu al-abrar cha Al-bahraniy uk245

alikubali na akamuahidi toba na uongofu na amali njema, akajua kwamba mnasibisho wa mwanzo ulikuwa ni dhambi na upotofu na amali mbaya, na hayo yako wazi wala isidhaniwe kuwa ni katazo kwa kauli yake: "anataka kuwa mzigo kwa watu" kwani kukataa kwake hakukua wazi pale alipozungumzia wema, na kama hakusudii tuliyoyasema basi ulinganisho ungekuwa ni fasidi, kwa hivyo inabainika kwamba jina hili halijazoeleka katika sharia, vipi ijuzu kumtaja mutasawif mahali hapa endapo haingii kiujumla halafu Imamu aseme anayoyasema? jee hii si kujinata kwa ujinga, ni wazi kwamba yeye ndiye mlengwa au ni mwenye nafasi kubwa na ulinganisho unalipa nafasi kubwa hilo la mwanzo[1]

[1] Arrisala al-ithna asheriya

# MSIMAMO WA IMAMU AL-RIDHA JUU YA MASUFI NA HUKUMU YAKE KWAO KUWA NI WATU WA UPOTOFU NA WAJINGA NA MWENYE KUWAPINGA NI SAWA KWAMBA AMEPIGANA JIHADI DHIDI YA MAKAFIRI PAMOJA NA MTUME ﷺ

Ameelezea Al-ardabiily ndani ya kitabu chake " Hadiyqat asshiya" kutoka kwa Abu Al-khatab kutoka kwa Imamu Al-ridha kwamba amesema "Hawi mtu mutasawif isipokuwa kwa ajili ya kuhadaa, au upotofu au upumbavu"[1]

Na katika riwaya nyengine kutoka kwa Abu al-qasim Jaafar bin Muhammad quwlawayh kutoka kwa Saad bin Abdillah kutoka kwa Ahmad bin Muhammad bin Issa kutoka kwa Alhusain bin Said amesema " Nilimuuliza Al-ridha kuhusu masufi, akasema hajiiti mtu mutaswifu ispokuwa kwa kuhadaa au upotofu au upumbavu au huenda mmoja wao amekusanya yote."[2]

---

[1] Hadiyqat alshiya uk 251

[2] Hadiyqat Al-shia

Anasema Alhur Al-amily katika kuielezea hadithi hii na vigawanyo vitatu vilivyotajwa (hadaa na upotofu na upumbavu) vinatubainishia kwamba tasawuf na mambo wanayosifikana nayo watu wake ni mambo ya uzushi na bidaa, na hii ndiyo sunna ya maadui wa maimamu, na atakaejinasibisha kwao ima atakua ni katika viongozi, hao watakuwa ni kundi la mwanzo, au katika wafuasi walioghururika na kudhihirisha uzuhudi wa viongozi hawa ni kundi la pili au kwa sababu ya upungufu na ufahamu mbaya na kutosheka na ujuu ujuu wa mambo huyu ni kundi la tatu, na kauli ya mkato ya wazi juu ya hawa ni ubatili wa makundi yote.

Imepokewa kutoka kwa Al-ridha kwamba amesema "Watakapotajwa masufi mbele ya mtu na akawa hakuwapinga kwa ulimi wake au kwa moyo wake huyo hayuko pamoja na sisi, na atakaewapinga ni sawa kwamba amepigana jihadi na makafiri pamoja na Mtume ﷺ na watu wake.

Alhur al-aamily ameeleza kuhusiana na riwaya hii kwa kusema " nasema kwamba katika maneno haya kuna usemi wa wazi kuwa kuwakemea masufi ni wajibu kwa namna itakavyowezekana na hii ni nyongeza ya dalili za ujumla zenye kuwajibisha kukemea maovu, pia zimo dalili za ukafiri wao kwa kule kutajwa kuwa wameshabihiana na makafiri, lakini inawezekana ikawa imekusudiwa kushabihisha kuwakemea wao kuwa ni kama kupigana jihadi na makafiri pamoja na kuwahukumia ukafiri, siyo kuwashabihisha wao na makafiri, na kwa hali zote mbili, hukumu ya wao kuwa ni makafiri ni jambo la lazima[1]

[1] Risalatu ithnaashiriya uk 32

# MSIMAMO WA IMAMU AL-HAADI JUU YA MASUFI NA HUKUMU YAO KWAMBA NI MANASARA NA WAMAJUSI WA UMMA HUU

Amesema Al-ardabiily katika kitabu chake "Hadiyqatu al-shia" kutoka kwa Muhammad bin Al-hassan bin Abu Al-khatab amesema; "Nilikuwa na Al-haady Ally ibin Muhammad عليه السلام kwenye msikiti wa Mtume ﷺ wakamjia kundi la watu wake akiwemo Abu Hashim Al-jaafary na alikuwa ni mtu mwenye fasaha na alikuwa na nafasi nzuri mbele yake, baadae wakaingia msikitini kundi la masufi wakakaa duara na kuanza kuleta tahlilati akasema, msikae pamoja nao hao ni wenye hadaa, hakika hao ni washirika wa shetani wenye kuharibu misingi ya dini, wanafanya zuhudi kwa ajili ya raha tu za miili yao, na wanakesha usiku kwa ajili ya kuwinda tu wanyama, wanashinda na njaa kwa ajili ya kupata rangi nyekundu (miili yao), hawaleti tahalilati ila tu kwa ajili ya kuwahadaa watu, wala hawapunguzi kula isipokuwa kwa ajili ya kuzuia vyungu, kufilisi nyoyo za wanawake wajinga, wanawazungumzia watu kuhusu mapenzi kumbe wanawaingiza mashimoni, nyiradi zao ni kucheza na kofi na nyimbo, hawawafuati isipokuwa wajinga, wala hawawaamini ila wapofu, na yeyote atakaewatembelea wakiwa hai au maiti ni kama kawasaidia Yazid na Muawiya na Abu Sufiyan, mtu

mmoja akasema kumwambia Imam hata kama wanakutambueni haki zenu? Akamtazama mtazamo wa ghadhabu, akasema wacha haya, atakaezikiri haki zetu hajatoka akilini mwetu wewe hujui kwamba; Wao ni kundi ovu, na masufi wote ni wapinzani wetu, na njia yao ni kinyume ya njia zetu na kua wao ni majusi wa umma huu, nao ni wenye kujaribu kuzima nuru ya Allah, na Allah anakamilisha nuru yake hata kama watachukia makafiri[1].

Anasema Alhur Al-aamily kuhusu riwaya hii, ''Laiti isingalipokewa hadithi nyengine zaidi ya hii yenye ufasaha na iliyojaa maana katika kuhadharisha dhidi ya masufi ingalitosha kwa bayana yake na kuonyesha upotofu wao, na imebainisha ufisadi wa njia yao kwa uwazi wa kutosha kabisa. Wala haikutofautisha baina ya wakubwa wao na wengine wakawaida bali wote wako katika njia mbovu, na kwamba maimamu wako tofauti nao na kwamba hao ni makafiri na wametoka katika uislam. Yote hayo yako wazi kwa wenye fahamu[2].

---

1 Hadiqat al-shia uk 603

2 Risaalatu Al ithna ashariya uk 29-30

# MSIMAMO WA IMAMU AL-ASKARY JUU YA MASUFI

Amesema Al-ardabiily katika kitabu chake "Hadiyqat al-shia" na Alhur Al-amily katika kitabu chake "al-risalatu al-ithnaashiria " kutoka kwa Al-askary عليه السلام, kwamba alizungumza na Abu hashim Al-jaafary, akasema "Ewe Abu Hashim utakuja wakati kwa watu, nyuso zao zitakua ni zenye bashasha na zinaonyesha bishara njema, lakini nyoyo zao ni zenye kiza, sunna kwao ni bidaa, na bidaa kwao ni sunna, muumini kwao hana heshima, na fasiki kwao ndie mwenye heshima, viongozi wao ni majahili madhalimu, na maulama wao wapo kwenye milango ya madhalimu wanawaendea, matajiri wao ni wezi wanawaibia mafakiri, na wadogo wao wako mbele, kila jahili kwao ni mjuzi na kila mjanja kwao ni fakiri, hawatofautishi baina ya mwenye ikhlasi na mwenye shaka, hawatambui kondoo baina mbwa mwitu, **Maulamaa wao ni watu shari wa viumbe vya Allah katika ardhi, kwani wao ni wenye kutegema falsafa na tasawuf,** wallahi ni watu wa kupinda na maharibiko, wanachupa mipaka kuwapenda maadui wetu na wanawakufurisha watu wetu na mawalii wetu.[1]

[1] Hadiyqatu aal-shia uk566 na al-thnaashiria

# IJMAI YA SHIA IMAMIYAH YA UBATILI WA MASUFI NA KUFURU YA WAFUASI

Wamewafikiana maulamaa wa shia imamiya zamani na hivi sasa juu ya ubatili wa tasawuf na ubaya wa watu wake, na wanasifiwa kwa sifa mbaya, na katika maulamaa walionukuu ijmai hii na kuichambua ni sheikh wao Al-hur Al-aamily katika kitabu chake "Al-risalat al-ithnaashira fiy rradi ala al-sufiya "[1]. Baada ya kutaja dalili za kiakili na riwaya kutoka kwa Mtume ﷺ zinazoelezea ubatili wa tasawuf, na ubaya wa watu wake, amekuja na sehemu ya nane ambayo amezungumza humo ijmai akasema.

Ya nane; Ijmai ya shia al-imamiyah, mapote yote yanakubaliana juu ya ubatili wa masufi, na kustahiki kujibiwa, tangu wakati wa Mtume ﷺ hadi zama hizi, na bado wanaendelea kuwakemea huku wakifuata maimamu wao katika hilo, na tayari umeshajua baadhi ya yaliyopokewa kutoka kwao, na yametajwa pia katika mlango wa mwanzo yenye ishara ya hayo, na yatakavyokuja maelezo yanayoonyesha hivo inshaallah, na kwa hivyo ishabainika wazi kwamba Maimamu wa kishia عليهم السلام wanaingia kwenye ijmai hii, hivyo hoja ya ijmai hii imeshadhi-

[1] Kwenye kitabu hichi tnanukuu mara kwa mara riwaya kuwapinga masufi

hirika na kujulikana usahihi wake, na inajulikana kwa elimu yenye yakini kua hiyo ndio hali ya shia al-imamiya kwa kila mwenye kuwajua na kusoma vitabu vyao, lakini licha ya hivyo bado imenukuliwa ijmai hii kutoka kwa kundi la maulamaa wao wakubwa, na wametoa kauli za wazi maulamaa wao bora, na utayaona majina yao inshaallah, na kuhusu kukubaliana maimamu wao na ijmai hii kuko wazi katika hadithi zilizotangulia na mfano wake, kiasi ambacho hakuna yeyote aliyewaita jina hili wala hakuna shia aliewanasibisha wao na jina hili. Na tambua kwamba jumla ya walionukuu ijmai hii ni Bwana mkuu Abu Al-maaly Muhammad bin Niimatilahi Al-husainy katika kitabu alichokiandika kuhusu makundi ya kidini, katika kuzungumzia masusfi amesema.''Wengi katika ahlusunna waljamaa wamewakataa masufi, na mashia wote wamewakataa mutasawifa, na wamenukuu toka kwa maimamu wao hadithi mbali mbali dhidi yao, mpaka akasema '' na shia wote wanaona kuwa masufi ni makafiri, na kwamba ni lazima kuwarudi kwa nguvu zote, mpaka wamekataza mtu kuitwa sufi, na wamepokea hadithi nyingi zenye maana hii kutoka kwa maimamu wao.

# MSIMAMO WA MAULAMAA WA KIIMA-MIYAH WALIOWARUDI MASUFI NA KU-WAITA MAKAFIRI NA WAPOTOFU

Baadhi yao ni:

Sheikh wao Ahmad bin Muhammad Al-adhrabaijany maarufu kwa Almuqadas Al-ardabiily (kafa mwaka 933 hijria)[1], amewahujumu masufi na akawaita kua ni washirika wa shetani, na waharibifu wa misingi ya dini, bali ni majusi wa umma huu.

Anasema Al-ardabiily katika kitabu chake "Hadiyqatu al-shia "Musiwafuate masufi kwani hao ni washirika wa shetani na waharibifu wa dini, wanafanya zuhudi kwa ajili ya raha za miili yao wanakesha usiku kwa ajili ya kuwazuga watu, mwenye kuwa pamoja nao ni kama kwamba amemfanyia ziara shetani, na ameabudia visivyostahiki (mizimu), na atakaemsaidia mmoja wao ni kama kwamba amemsaidai Yazid na Muawiya na Abu Sufiyan.

Hajatoshelezeka na haya tu, bali amesema kuwa wao ni majusi wa umma huu, akasema " Masufi ni manasara na majusi wa umma huu, na ni wenye kupigania kuzima nuru ya Allah

---

1 Ahmad bin Mohammad Al-adharbaijany maarufu kwa Al-muqadsa Al-ardabily

lakini Allah anakamilisha nuru yake hata kama watachukia washirikina.

Na anawashambulia zaidi watu wa alhlul-ilhad katika masufi wa zamani, mfano wa Muhidin bin Arabiy na Abdulrazak Al-kashany na sheikh Azizi Alnasafy na anawaita **makafiri na wazandiki.**

Sheikh Almufiid, anasema kuhusu masufi kuwa ni watu wa kuhalalisha kila kitu (al-ibahiya) bali ni makafiri na wazandiki.

Na katika masheikh muhimu wa Al-imamiya waliotunga kuhusu kuwarudi masufi ni sheikh Almufiid, anasema Alhur Al-amily ''Sheikh Almufiid Muhammad bin Muhamad bin Nuuman siri yake itakaswe, ametunga kitabu dhidi ya masufi watu wa Alhallaaj, na kila alietunga kitabu kuwarudi masufi basi amenukuu kutoka kitabu hicho na wamekitaja kitabu hicho katika kuelezea historia yake kama ilivyo katika faharisi za Al-najaashi na na Alsheikh na wengine. Baadhi ya maulamaa wetu wamesema kwamba Sheikh Almufiid amesema katika kitabu hicho (dhidi ya Al-hallaaj). Tambua kwamba mwanachuoni huyu mara nyingi anadai uimamu kauli zake za Dhahiri ni tamu lakini batini yake ni vitendo vibaya, anatangaza uchamungu na imani lakini anaficha moyoni kufuru na uadui, anakula vya dunia kwa jina la dini, anaingiza shubha kwenye nafsi za waumini dhaifu, na anawapinga na kuwakufurisha aali-bayt, tulipoona kujiingiza watu wa alhallaaji katika kuwaghururi wafuasi dhaifu katika firqatu alnaajiya (kundi okovu), tukajikita katika kuzuia upotofu wao na kurudi kauli zao ili watu wetu wasije wakadanganyika nao wakachupa mipaka na kua mbali na njia ya kuokoka[1]

Na katika aliyoyasema Al-mufiid kuhusu Masufi: ''Na

[1] Arisalat al-ithnaashiriya

wafuasi wa Al hallaaj ni kundi katika makundi ya masufi nao ni watu wa alhululiya na al-itihadiya, wala hakuwa Al-hallaaj anajidai kudhihirisha ushia, japokuwa Dhahiri yake ni mutasawif, watu hao ni makafiri na wazandiki, wanadai kudhihirisha kila kundi ndani ya itikadi zao na wanadai kwamba Hallaaj ana miujiza na makarama (madai ambayo ni batili), wanafuata njia za al-majusi katika kumdaiya alzaraadishti (Zorasta) miujiza, na wanafuata njia za manasara katika kuwadaiya miujiza watawa wao. Na manasara na majusi wako karibu zaidi na ibada kuliko masufi, nao (masufi) wako mbali zaidi na sharia na kuzifuata kuliko hata manasara na wamajusi.

Mwanachuoni wao mkubwa wa hadithi Abu Jaafar Baabawayhi[1], amekwenda mbali zaidi katika kuwapinga masufi,

Katika viongozi wao aliekwenda mbali sana katika kuwarudi na kuwataja vibaya masufi ni Sheikh wao Abu Jaafar bin Baabawayhi, anasema Alhur Al-amily kuhusiana nae "Ni sheikh mkubwa kiongozi wa maulamaa wa hadithi Abu Jaafar Baabawayhi, na umeshajua kwamba amezaliwa kwa dua za Sahib Al-zaman (alayhi salam) na fadhila zake ni nyingi mno hata kuhesabika, na amewarudi sana katika vitabu vyake vya itikadi na hadithi mfano "Uyun al-akhbaar" na "maani al-akhbaar" na "Tawhid wa al-ilal" na amepokea hadithi nyingi katika kuwarudi[2].

Al-majlisy[3] alikua mkali katika kuwapinga masufi na kuhadharisha dhidi ya minhaji zao. Anasema Almajlisy katika

1 Mohmad bin Ali bin Hassan bin Mussa bin Baabawayhi Al-qummiy mashuhuri kwa Sheikh A-saduqi amezaliwa 306

2 Arrisalat al-ithnaashiriya uk48-49

3 Sheikh Mohammad Baaqir bin Alsheikh Mohammad taqiy Almajlisy Al-aaafahaniy (1111hijria 1699)

kitabu chake Al-aqaaid (Iitiqadat almajlisy): ‘‘Kundi la watu wa zama zetu wamefanya bidaa kuwa ni dini, wanamuabudu Allah kwa bidaa na wanajiita masufi, wamefanya utawa ni ibada wakati ambapo Mtume ﷺ amekataza hilo, na ameamrisha kuoa na kuchanganyika na viumbe, na kuhudhuria mijumuiko, na kukusanyika na waumini, na kulingaliana kheri baina yao, na kufundishana elimu na ibada, na kutembelea wagonjwa na kufanyiana ziara na kuwakidhia mahitajio yao, na kulingania maamrisho na kukatazana maovu, na kusimamisha sharia za Allah, ama utawa waliouzusha unapelekea kuacha faradhi na sunna, na katika utawa huo wamezusha ibada mpya, kama dhikri ambayo ni amali maaulum kwa umbo maalum wala haikupokewa maandiko wala athari yoyote bila shaka amali kama hizi ni haramu, na amesema Mtume ﷺ kila bidaa ni upotofu na kila upotofu ni njia ya motoni, Pia na dhikri hii ya wazi wanayoiimba kwa mashairi, kwa sauti kama sauti za mapunda, wanamuabudu Allah kwa makofi na makelele, na wanadai hakuna dhikri mbele ya dhikri mbili hizi za bidaa, na wanaacha sunna zote, wanasali sala za faradhi mfano wa midonoo ya jogooo na kunguru na kama sikuchelea maulamaa wangeliziacha kabisa.

Allah awalaani hawatosheki na bidaa tu lakini wanageuza dini, na wanadi wahdatu-lwujud na tafsiri mashuhuri ya kauli hizi inayotoka kwa masheikh wao ni kufru ya kumkufuru Allah Mtukufu, wanadai fikra ya al-jabriya (kukosa hiari), kuondokewa na wajibu wa ibada na mambo mengine ya ufisadi na upuuzi.

Jihadharisheni ndugu zangu, na hifadini dini yenu na wasiwasi wa mashetani hawa na wito wao, na msihadaike na uongo wao ambao nyoyo za watu majahili zimekamatana nao,,.

Niimatullah Aljazairy[1] anasema kuhusu masufi kwamba ni watu waliotoka nje ya njia ya haki, na anatilia mkazo Niimatullah kwamba tasawufi ni njia ya mafilosofi na wazandiki na makafiri, na anasema katika kitabu chake "Al-anwaar alnuumaniya", chini ya anuani " kiza kikubwa katika kubainisha masufi na nawasib (maadui wa aalil bayt) kwamba jina hili la tasawuf lilikuwa linatumiwa na mafilosofi waliopotea njia, baadae wakalitumia wazandiki[2]

Shihabu Al-diyn Al-najafy Almar-ashy anasema kuhusu masufi na tasawuf kuwa ni msiba mkubwa kwa uislam. Anasema Seyyid Shihabu al-diyn Alnajafy katika kitabu chake "Ihqaaq al-haq". "Kwangu mimi matatizo ya sufiya juu ya uislam ni matatizo makubwa zaidi, uislam umeingia madowa na kutetereka jengo lake," Baada ya utafiti wa kina na kuzifuatilia dhamiri za maneno yao, kujionea mambo yao yaliyofichikana baada ya kukaa na viongozi wao, imenibainikia kwamba maradhi yalijipenyeza kwenye dini kutoka watawa wa manasara, yakabebwa na watu wa chini mfano wa Al-hassan Al-basry, Al-shibily, Maaruf, Twauus, AL-zuhry, Juneid na wengineo, baadae yakajipenyeza kwenye ushia, mpaka wakapanda cheo na bendera yao kupepea, wakawa hakuna walichobakisha katika misingi ya dini, wakapotosha tafsiri ya nususi za kitabu na sunna, na wakaenda kinyume na mambo ya fitra na akili wakashughulika na "wahdatuul-wujud", na wakajiundia namna maalum ya kuabudu na wakaendelea kujishughulisha na nyiradi zilizojaa kufuru na batili.."[3]

---

1 Seyyid Niimtullah bin Abdallah bin Mohammad Alhusayn Almuusawy Aljaziry (1050 h 1640h Alsabaghiya kijiji cha Algeria

2 Tazama Al-anwaar al-nuumaniya uk 193

3 Ihqaaq al-haq uk 183-185

Muhammad bin Tahir bin Muhammad bin Hussein Al-shirazy Al-najafy Alqumy, anawahukumia masufi kuwa ni makafiri na wanafiki. Muhammad bin Tahir Al-shirazy (amekufa mwaka 1098 h) ni mmoja wa wakosoaji wakubwa wa tasawuf na wafuasi wake, anasema Daktari Muhsin Jahankiiry, mwalimu wa falasafa katika chuo kikuu cha Teheran katika kitabu chake (Muhidin bin Araby), ",,,,,,,, Alikuwa ni mwenye elimu juu ya itikadi za watu wa tariqa, kati ya hizo ni kauli ya wahdatul-wujudi, na akaipinga kwa kila hali na kuikataza akasema haiendani sawa na kauli za saahibu sharia, hasa kauli za Ibn Arabiy.

Vile vile amepondaponda misingi mingi ya tasawuf kama vile wahdatul-wujud na matawi yake, akawakufurisha wote wanayoi-kubali, bali akasema kuwa kufuru yao ni ya wazi kuliko kufuru ya mayahudi na manasara.

Al-marjii Alshirazy anaona kufuru ya masufi ni ya wazi kuliko kufuru ya mayahudi na manasara.

Hapana shaka wafuasi wa njia hii mbaya, hata wakijidhirisha katika guo la uislam na wakajificha kwenye unafiki, lakini kufuru yao kwa wenye akili ni ya wazi kuliko kufuru ya mayahudi na manasara, kwani wanakataa Mughayarat Alkhaliq wa lmakhluq (Utofauti wa Muumba na kiumbe) ambao ni jambo la dharura katika dini zote.."[1] Na akaendelea Ashiraazy kutaja kauli mbali mbali za Ibn Araby za kufuru na kuzirudi kisha akahitimisha kwa kusema "kuna dalili za wazi juu ya kufuru ya Ibn Arabiy kwa kauli zote hizi za kikufuru, na ambae hamkufurishi anaesema kauli hizi basi na yeye ni kafiri, hana dini wala hayumo kwenye yakini,

Na ameongezea daktari Jahankiiry "na kwa ufupi alikuwa

[1] Tuhfatu al-akhbar Cha Al-shirazy uk 58

sheikh al-islamy Al-shirazy, katika wapinzani wakuu wa Ib Araby katika ulimwengu wa kishia, amekuwa wazi katika kupiga vita bila kurudi nyuma na alikuwa muwazi dhidi yao, wakati mwengine bila hata ya dalili za kielimu, na akampa wasifu wa upotofu, uzushi, ujinga, kafiri kuliko Yazid na hana dini, pia akapinga misingi yake mengine ya tasawuf pia na kuyafanya ni katika jumla ya mambo yanayo kwenda kinyume na misingi ya dini na Madhehebu ya Imaamiya.

Al-muhaqiq Muhsin bin Baydaaraf anawahukumu wenye kujinasibisha na tasawuf kuwa ni makafiri na ni wazandiki.

Hakukhitilafiana Muhaqiq wa kitabu ''Ilmu alyaqiyn fiy usul aldiyn'' na watangulizi wake wawili miongoni mwa masheikh wa al-imamiyah, akasema kujinasibisha na watu wa tasawuf ni sawa na kujinasibisha na makafiri na wazandiki anasema,''Hakika kujina-sibisha na tasawuf ni sawa na kujinasibisha na kufuru na ilhaadi na uzandiki, na jambo hili limewapelekea maulamaa wengi wa leo kuandika vitabu dhidi ya masufi na kuwahukumia ukafiri na rida.''

Almuamam Allibnaany wa zama hizi Muhammad Jamiil Hamoud Al-aamily amebainisha msimamo wa Al-imamiya juu ya masufi, imekuja katika tovuti yake suala la falsafa na al-irfaani akajibu hivi; ''Kwa jina la Allah, falasafa na al-irfaan ni aina mbili za tasawuf, na tasawuf ni katika bidaa za wenye kwenda kinyume nasi, na msimamo wa maimamu wetu ni kuikataa na kuipinga tasawuf na falsafa, kwa sababu ya hatari yake kwani tasawuf pamoja na al-irfaa huwepesisha njia zinazodai mtu kufikia kwa Allah kwa malengo mepesi na kwa daraja za kuundaunda, ikiwa kwa mwanchuoni, mtu jahili, hodari au pocho, kwa sababu ya mambo ya kufunuliwa na kupata elimu ya moja kwa moja (ilmu ladunny), ambazo wanadai kufunuliwa nazo na zinamrahishia mtu kila kitu, na njia hii iliyo

nyepesi wanapata wenye tamaa na wavivu yale wanayoyatamani bila ya mashaka na tabu, na bila ya kukesha au kujitahidi kimawazo kutafuta au kusoma miaka kadha kwa ajili ya kupata maarifa ya hukumu za Allah, na kujua uhakika wa aya za Allah katika Quran na Sunna. Na hali hii inafungua njia kwa masheikh wao na wanafunzi wao kujidai kwamba wao ni wajuzi wakubwa na wenye hekima na maulamaa wakubwa ambao hastahiki mtu kuwauliza jambo au kuwataka dalili, kwa sababu kufunguliwa (al-kashf) ni sawa na bakora ya Mussa na pete ya Suleiman na buraqu wa Mtume ﷺ.

Kudai al-irfaan na tasawuf vinafungua njia inayopelekea kutokua na haja ya imam maasum (asiekosea), kwani sheikh wa kisufi na al-irfaan anapodai kupata maarifa kupitia njia ya kufunuliwa (alkashf) hii inafungua uwanja wa mashirikiano ya kielimu baina yao na maasum, na jambo hili linapelekea kutokuwa na haja nae na badala yake watu watawafuata masheikh wa kisufi ambao watawaelekeza katika kupata al-kashfu na al-shuhud (kufunuliwa mambo).

Istilahi ya Al-irfaan ni istilahi mpya, wameitumia wanachuoni wa kisufi mfano Ibn Araby na Abu Yazid Albustaamy na wengineo, badala ya istilahi ya al-tasawuf, yote ni kwa sababu ya kutambua kwamba mashia hawataingia na kufuata njia zao, kwa sababu ya utiifu wao kwa maimamu wao, waliowakataza kujikurubisha na njia yao,,, pamoja na ghururi ya baadhi ya wanaojidai utaalamu katika masufi ambao waliwadanganya baadhi ya wanafunzi dhaifu wanaosoma taaluma za dini kwenye vituo vya kielimu hasa hasa Iran, hivyo wakaunda kundi la kuitangaza njia yao ya Al-irfaan na kuwalingania watu."[1]

---

1 Tazama fatwa kwa ukamilifu kwenye (Markaz al-atira al-tahira) www. Aletra.org

# HAIJUZU KUJINASIBISHA NA TASAWUFI ISIPOKUWA KWA HALI YA KUFANYA TAQIYA[1]

Licha ya ukosowaji wote na ukufurishaji na ubidaa waioudai mashia imamiya dhidi ya masufi, na kujiita kwa jina lao, lakini wamejawizisha kujinasibisha na masufi katia hali ya taqiya. Imekuja katika kitabu cha "Hadiyqat al-shia",kutoka kwa Al-ridha " Hajinasibishi mtu na tasawuf isipokuwa kwa hadaa au upotofu au ujinga, ama atakaejiita sufi kwa taqiya hatakuwa na dhambi.[2] Na katika njia nyengine amezidisha kwa kusema; "Atakaejiita sufi kwa taqiyya hatokua na makosa".

Anasema Al-ardabiily "Na alama yake ni kutoshelezeka na kujiita tu asiamini chochote katika itikadi yao batili"[3].

---

1 Taqiya katika lugha ni kufanya hadhari na ktika ushia ni kudhihirishi kinyume na yaliyomo moyoni, taqiya ya kisheria ni masuala ya furuu na sio usul na mtu akiacha sio kosa, lakini kwa mashia ni usulu wa dini na lazima na hana dini asiekuwa na taqiya, kwa shia ni lazima kwa mukalaf katika kauli zake na vitendo, ndio maana shia ni waongo sana zamani na hivi sasa kwani uongo wameufanya ni dini Ama taqiya kisheria inawezekana tu katika dharura mfano kulazimishwa kufanya jambo, au katika muamala wa makafiri tu, kwa zaidi soma kitabu cha daktari Naser Alqefary "usul madhhabu al-shia

2 Hadiyqat alshia uk 251

3 Hadiyqat alshia uk 251

Anasema Alhur Al-amily akielezea riwaya hii, nasema “ Hapa panazidi kuzuia kujiita (sufi) na kutangaza ubatili wao katika baadhi ya itikadi zao au zote, kwa sababu neno **"batili"** ni sifa ya neno (akaaid) itikadi, na kama neno **"batili"** ni la takhsis basi kauli ni ya mwanzo, na kama ni la kupambanua basi kauli ni ya pili. Na hakuna shaka kwamba taqiya haipelekei kwenye kuafikiana katika itikadi, kwa sababu mpinzani haiyoni, na taqiya itakuwa ni haramu kama hakuna ulazima wa kuifanya bali kinachopasa ni kutokuyaamini mambo yao na kwamba taqiyya isiyo na lazima itakua ni haramu, na ndio maana hazikutajwa aamaal kwa sababu inawezekana kukawa na haja ya taqiyya kuzidhihirisha.

# MWISHO

Inakubainikia ewe ndugu yangu msomaji, ukweli wa msimamo wa shia imamiya dhidi ya masufi, kwa haya tuliyokuonyesha katika maneno ya maimamu wao maasum, pamoja rejea zao na maulamaa wao wa zamani na wa zama hizi

Masufi kwa mujibu wa misimamo ya kishia ni

- Makafiri kuliko mayahudi na manassara.

- Ni majusi wa umma huu.

- Ni watu wa motoni.

- Ni kundi lilopotea na lililolaaniwa

- Jina la tasawuf lilikuwa linatumiwa na makundi ya mafilosofi na watu waliopotea, baadae likatumiwa na makundi ya wazandiki maadui wa aalil-bayt.

Hawa ndio masufi kwa mtazamo wa shia, na hizi ndizo hukumu zao.

Jee tutahadaika baada ya leo na kauli zao za kulingania umoja?

Jee tutawasadiki kwamba wanawapenda ahlu sunna, Wawe masufi au wengineo?

Haitotuhadaa tena baada ya leo taqiya yao, wala hayatotughururi maneno yao matamu, wala hatutakuwa pamoja nao maadam hawataachana na itikadi zao na kuitakidi itikadi ya Quran na Sunna sahihi na kuacha kufuata itikadi za upotofu.

Inambainikia kila mwenye akili, kwamba shia wa sasa, ni wafuasi wa waliowatangulia, wote ni sawa hakuna tofauti ya waliopita na wa leo, Allahuma isipokuwa kwa kiasi cha amali kwa taqiya.

وصلى الله وسلم على نبينا محمد وعلى آله وصحبه أجمعين

# ORODHA YA VITABU MUHIMU DHIDI YA SHIA

- ❑ فتاوى شيخ الإسلام ابن تيمية.
- ❑ منهاج السنة لشيخ الإسلام ابن تيمية.
- ❑ الملل والنحل للشهرستاني.
- ❑ الفرق بين الفرق للبغدادي.
- ❑ مقالات الإسلاميين للأشعري.

*** من الكتّاب المعاصرين:**

- ❑ **جميع مؤلفات الشيخ إحسان إلهي ظهير.**
- ❑ **(مسألة التقريب)** للشيخ د. ناصر القفاري.
- ❑ **(أصول مذهب الشيعة الاثني عشرية)** للشيخ د. ناصر القفاري.
- ❑ **جميع مؤلفات الشيخ محمد مال الله.**
- ❑ **(بذل المجهود في مشابهة الرافضة لليهود)** لعبدالله الجميلي.
- ❑ **(حتى لا ننخدع)** لعبدالله الموصلي.
- ❑ **(الشيعة الاثنا عشرية وتكفيرهم لعموم المسلمين)** لعبدالله السلفي.

- **(من قتل الحسين)** لعبدالله بن عبدالعزيز.
- **(البرهان في تبرئة أبي هريرة من البهتان)** لعبدالله الناصر.
- **(الانتصار للصحب والآل)** للدكتور إبراهيم الرحيلي.
- **(كشف الجاني محمد التيجاني)** للشيخ عثمان الخميس.
- **(بل ضللت في رد أباطيل التيجاني)** للشيخ خالد العسقلاني.
- **(مع الاثني عشرية في الأصول والفروع)** للدكتور علي السالوس.
- **(تبديد الظلام وتنبيه النيام على خطر التشيع على المسلمين والإسلام)** للشيخ سليمان الجبهان رحمه الله.
- وغيرها كثير، وهذا على سبيل الاختصار لا الحصر.

## MITANDAO MUHIMU AMBAYO TUNASHAURI KUPERUZI KATIKA KUWARUDI RAFIDHWA ITHNA ASHARIA

http//:www.dd-sunnah.net

http//:www.fnoor.com

http//:www.albrhan.com

http//:www.wylsh.com

http//:www.khomainy.com

http//:dhr١٢.com

http//:www.albainah.net

http//:www.ansar.org

http//:www.almanhaj.com

http//:www.isl.org.uk

http//:www.al-mhdi.com